



# Ofisi ya Taifa ya Takwimu

Simu: +255 26 - 2963822  
Nukushi: +255 26 - 296382  
Barua pepe: sg@nbs.go.tz  
Tovuti: www.nbs.go.tz

Barabara ya Jakaya Kikwete  
S. L. P. 2683  
**Dodoma**  
**TANZANIA**



Kumb. Na. BA.275/376/01/127

TAARIFA KWA UMMA

Tarehe: 8 Septemba, 2021


## MWENENDO WA VIASHIRIA VYA KIUCHUMI VYA MUDA MFUPI, JANUARI - JUNI, 2021

Mwenendo wa viashiria vya kiuchumi umeendelea kuimarika licha ya kuendelea kuwepo kwa changamoto za UVIKO-19.

### a) Idadi ya Watalii

Idadi ya watalii imeendelea kuongezeka ambapo kati ya Januari hadi Juni 2021, kiwango cha watalii walioingia Nchini *kiliongezeka kwa asililima 4.5* ikilinganishwa na *kiwango hasi cha asilimia 43.6* kipindi kama hiki mwaka 2020. Idadi ya watalii walioingia Nchini mwezi Juni 2021 *walikuwa 57,689* ikilinganishwa na *9,671* walioingia Nchini mwezi Juni 2020.

### Idadi ya Watalii walioingia nchini: Januari - Juni 2018 - 2021




Chanzo: Idara ya Uhamiaji

Idadi kubwa ya watalii walioingia Nchini katika kipindi hicho walitoka **Urusi**. Mwenendo huu unaashiria kuendelea kuimarika kwa sekta ya utalii.

### b) Uzalishaji wa Saruji

Uzalishaji wa saruji umeendelea kuimarika ambapo ukuaji umeongezeka kwa *kiwango hasi cha asilimia 0.6* kutoka *kiwango hasi cha asilimia 5.1*.

### Uzalishaji wa Saruji: Januari - Juni, 2018 - 2021




Chanzo: Viwanda vya Saruji

### c) Huduma za Mawasiliano: Januari - Juni, 2018 - 2021

Shughuli nyingi za kiuchumi za huduma ziliathiriwa na UVIKO-19 isipokuwa huduma za mawasiliano ambayo imeendelea kuongezeka kutoka dakika za kuongea bilioni 31.3 kipindi cha Januari hadi Juni mwaka 2019 hadi dakika bilioni 42.9 kipindi kama hicho mwaka 2021.

### Muda wa Kuongea Katika Dakika: Januari - Juni, 2018 - 2021




Chanzo: TCRA

Matumizi makubwa ya huduma wakati wa athari za UVIKO-19 yalichangia ongezeko hili. Mathalani, katika kipindi hiki tumeshuhudia uendeshaji wa mikutano kwa kiwango kikubwa kwa njia ya video.

### d) Uzalishaji wa Nishati ya Umeme

Mwenendo wa uzalishaji wa nishati ya umeme umeendelea kuwa imara ambapo uzalishaji umeongezeka kutoka saa za kilowati milioni 3,478 kipindi cha Januari - Juni mwaka 2018 hadi saa za kilowati milioni 4,053 kipindi kama hicho mwaka 2021.

### Uzalishaji wa Umeme: Januari - Juni, 2018 - 2021



Chanzo: TANESCO

**Imetolewa na Ofisi ya Taifa ya Takwimu**  
**DODOMA**